

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Anuani ya simu "ELIMU"  
Simu: 026 296 35 33  
Barua pepe: [info@moe.go.tz](mailto:info@moe.go.tz)  
Tovuti: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)



Chuo cha Masomo ya Biashara na  
Sheria,  
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),  
Jengo Na. 10,  
S. L. P. 10,  
40479 DODOMA

Tarehe: 4 Mei, 2018

## TAARIFA KWA UMMA

Kumekuwa na taarifa za upotoshaji ambazo zinasambaa kwenye mitandao ya kijamii, ambazo zinaonesha dosari na makosa katika vitabu. Mojawapo ni picha inayoelezea viungo vya mwili wa mwanadamu na nyingine iko katika Kitabu cha Kiingereza chenye maneno yanayosomeka "*The Big City of Tanzania*".

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapenda kuutarifu umma kuwa kitabu kinachosambazwa kinachoelezea viungo vya mwili wa mwanadamu si chapisho la Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) na wala si miongoni mwa vitabu ambavyo vimesambazwa kwenye shule. Kitabu hicho hakina uhusiano wowote na wala hakifanani na vitabu ambavyo vimechapishwa hivi karibuni na TET.

Aidha, kuhusu kitabu cha Kiingereza, hilo ni chapisho la mwaka 2016 ambalo limefanyiwa marekebisho katika chapisho la mwaka 2018.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inawasihi watanzania kupuuza taarifa hizo ambazo siyo za kweli na zina nia ya kupotosha na kuleta usumbufu kwa jamii. Wizara pia inatumia fursa hii kuwakumbusha wananchi kuzingatia Sheria za Matumizi ya Mitandao na kutambua kuwa kutoa taarifa za uongo ni kosa la jinai.

Imetolewa na:

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Mwasu Sware'.

Mwasu Sware

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

04/05/2018